

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'**



Unapojibu tafadhali taja:-

Kumb.NA.HAN/DC/E.2/1/VOLL.II/50

21.02.2022

TANGAZO LA NAFASI MOJA (1) YA KAZI

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Hanang' imepata kibali cha ajira mbadala chenye **Kumb. Na. FA.170/448/01"A"/74** cha tarehe **17 Novemba, 2021** kwa ajili ya kuajiri mtumishi mmoja (1) kujaza nafasi ya **Mtendaji wa Kijiji III**.

Hivyo,Watanzania wote wenye sifa zilizoorodheshwa katika Tangazo hili mnatakiwa kuwasilisha maombi ya kujaza nafasi hii.

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA III – NAFASI 1

SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji awe na Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika Moja ya Fani zifuatazo:-

- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

MAJUKUMU

1. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
2. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
3. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
4. Katibu wa Mikutano ya Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
5. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu za Serikali.
6. Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
7. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitalaam katika Kijiji.
8. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji.
9. Mwenyekiti wa Kikao cha wataalam waliopo katika Kijiji.
10. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na Migogoro ya Wananchi.
11. Kusimamia Utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji
12. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

MSHAHARA:

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia Waraka wa mishahara ya Watumishi wa Serikali ambao ni TGS. B

MAELEKEZO YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- i. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenye umri kati ya miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- ii. Maombi yaambatishwe na taarifa ya maelezo binafsi (Curriculum vitae) ya muombaji ikionesha wadhamini watatu na taarifa zao sahihi, namba za simu za muombaji na wadhamini, cheti cha taaluma, cheti cha kidato cha nne, cheti cha kuzaliwa, na picha mbili (2) passport size (ziandikwe majina kwa nyuma).
- iii. Testimonial na provisional statement of results, hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita **HAVITAPOKELEWA**.
- iv. Waombaji waliostaafu / kustaafishwa au kuacha kazi katika Utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kwa kibali cha Katibu Mkuu kiongozi.
- v. Muombaji atakayewasilisha taarifa na sifa za kughushi atachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa utaratibu.
- vi. Barua zote ziandikwe kwa mkono kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.
- vii. Waombaji waliopo katika Utumishi wa Umma wapitishie barua zao kwa waajiri wao.
- viii. Muombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
- ix. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatishe cheti cha ulinganifu (equivalent certificate) kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania.
- x. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **07/03/2022** saa **9:30 Alasiri**.
- xi. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta au barua pepe (Email) ded@hanangdc.go.tz

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA,
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG,
S.L.P 2,
KATESH – HANANG’.**

NB: Maombi yatakayotumwa kwa mkono hayatapokelewa

Elizabeth J. Lussingu

**ELIZABETH J. LUSSINGU
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
HANANG’
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA
HANANG**